


# YUSUFU AKIKUTANA

## NA NDUGUZE

 ...nikiwa na sauti ya kutosha kuongea kidogo. Nami nimepwelewa na sauti kwa muda. Na—na, asubuhi ya leo, nina mafua makali; inaonekana, kila mara tu ninaposhuka huku, kwa namna fulani, moja kwa moja kwenye bonde hili. Jana nilikuwa nikizungumza na baadhi ya ndugu tulipokuwa juu ya vilima huko New Albany, na tukatazama chini huku. Nikasema, “Hiyo hapo sababu yake, pale pale.” Ni ukungu tu unaoning’inia hapa juu, na mji mzima kufunikwa na kitu kama uchafu. Na mara ninapokuja katika eneo hili, mara tu ninaposhuka huku, huo hapo unaenda, mnaona, tena, punde tu ninapoingia. Loo, inanibidi kuchukua hema na kupanda juu ya kilima, mahali fulani, na kupiga kambi. Maana, sisi ni wasafiri tu na wageni, kwa vyovyote vile, sivyo? “Tukiutafuta Mji ambao Mwenye kuujenga na Mwenye kuubuni ni Mungu.” Huo ndio tunaoupenda. Sasa tuna baadhi. . .

2 Kabla tu ya ibada, asubuhi ya leo, na kabla ya mafundisho ya shule ya Jumapili, tuna ku—kuwekwa wakfu kwa watoto wachanga. Na ndugu yangu ana mtoto ambaye anataka awekwe wakfu kwa Bwana; ndugu yangu, wa kimwili. Na labda, baadhi yenu akina mama na baba hapa mna mtoto mdogo wa kuwekwa wakfu. Sasa, mara nyingi, katika Biblia. . .

3 Nasi tumekuwa na migawanyiko mingi makanisani, kwa sababu ya nadharia mbalimbali juu ya ubatizo wa watoto wachanga, na kadhalika. Na, sasa, wale wanaowachukua, na kuwanyunyizia kwa ubatizo wa watoto wachanga, hiyo ni kulingana na vile mnavyotaka kuwaweka wakfu. Lakini, jambo hilo lote linajumuika katika kitu kimoja, kuwekwa wakfu kwa Bwana. Mnaona? Na sasa. . .

4 Kwa sababu, mtoto mchanga, kuhusu dhambi, hana. Yesu alikufa apate kuondoa dhambi za ulimwengu. Naye huyo mtoto mchanga hajatenda dhambi, ila tu. . . Ni mwenye dhambi. Amezaliliwa katika dhambi. Lakini Kristo alipokufa pale Kalvari, aliziondolea mbali dhambi za ulimwengu, na mtoto mchanga hawajibiki mpaka aufikie umri wa kuwajibika. Basi mtoto yeyote mchanga, haidhuru wazazi wake ni watenda dhambi jinsi gani, mara afapo, anaenda moja kwa moja mikononi mwa Kristo, mnaona, kwa sababu Yeye alilipa ile gharama. Haidhuru kama ni mtoto mchanga aliyezaliwa katika dhambi, na kwa uzinzi ama chochote kile, haileti tofauti hata kidogo, mtoto huyo yuko salama pamoja na Kristo kwa sababu

alikufa apate kuziondoa dhambi za ulimwengu. Na wakati—wakati anapokuwa mzima vya kutosha sasa, ambapo ametenda dhambi ya kibinafsi, basi hana budi kuyatubia yale aliyofanya. Ila hana dhambi ya kibinafsi mpaka awe mzima vya kutosha kutenda dhambi, kujua mema na mabaya. Lakini, sasa, sisi daima tunajaribu kukaa karibu tu na Biblia juu ya mambo haya, kadiri tujuavyo.

<sup>5</sup> Sasa, hakuna Maandiko katika Biblia, ya kuwanyunyizia watoto wachanga. Kitu pekee tunachopata... Ama, hakuna ubatizo wa watoto wachanga katika Biblia, kwa namna yoyote. Mahali pekee tunapoweza kupata, palipoandikwa hapa katika Maandiko, kwamba Ye... “Walimletea Yesu watoto wachanga, Naye akawachukua mikononi Mwake na kuwabariki, na kusema, ‘Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa maana walio mfano wa hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.’”

<sup>6</sup> Sasa, kwa kuwa, sasa, kwa kuwa Yeye amekwenda kwa Mungu, na kuketi mkono wa kuume, leo hii, katika mwili Wake wa kawaida, na kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Naye ameliagiza Kanisa Lake kwenda ulimwenguni kote na kuendeleza kazi alizoanza hapa alipokuwa hapa duniani, yaani, kuihubiri Injili, kuwaponya wagonjwa, na kuwaweka wakfu watoto, na kadhalika. Kwa hiyo, wapendwa wanaombwa kuwaleta watoto wao kwa Bwana, kwa kumpa mchungaji wao, mikononi mwake. Naye anawainua, kwa imani, kwa Kristo, na kumwomba Kristo awabariki.

<sup>7</sup> Na, kwa hiyo, endapo unaye mtoto ambaye—ambaye hujamweka wakfu kwa Bwana, na ungetaka kumleta huku dada yetu akipiga kinanda, *Waleteni Ndani*, nasi tunaweza kuuimba. Ni wangapi wanaoujua huo wimbo wa kale, *Waleteni Ndani*? Basi hiyo ni sawa. Sasa, Bw. na Bibi Henry Branham watamleta mtoto wao. Na wengine wowote walio na wengine wanaotaka kuwaleta, vema, waleteni kuku huku wakati huu sasa wapate kuwekwa wakfu. Vema.

Waleteni ndani, waleteni ndani,  
Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;  
Waleteni ndani, waleteni ndani, (...?...) )

<sup>8</sup> Ninataka kuwaonyesha Branham mwingine mdogo, mtoto Mary Ella Branham. Ni binti wa ndugu yangu na mke wake mpendwa. Kwamba, wamejitokeza asubuhi ya leo, kanisani, kumtoa huyo mtoto, maisha yake, wamrudishie Mungu, Yule aliyewapa.

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

<sup>9</sup> Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, anayesimama hapa mbele yangu leo, ni ndugu yangu mwenyewe katika mwili, na bibi-arusi wake, mkewe. Nawe umeyabariki sana makazi yao na maskini Mary Ella huyu, kuwapa furaha katika siku zilizo

mbele yao. Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya kumbukumbu lao la mahali huyu mtoto mchanga alipotoka, na kumleta leo kanisani, wapate kumrudisha Kwako. Na sasa ninakabidhi huyu mtoto mchanga Kwako, katika mikono ya imani, na kukuomba umbariki huyu mtoto ninayemshika. Pia jalia aishi na kukua. Na kama Yesu akikawia, jalia awe mtumishi Wako, kukutumikia Wewe.

<sup>10</sup> Wabariki baba na mama yake. Na, Mungu, jalia kwamba Roho Wako Mtakatifu atawaongoza katika safari ya maisha. Na siku moja, wakati safari hii ya duniani itakapokwisha, jalia familia yote kubwa ikusanyike pamoja katika Utukufu. Tujalie, Bwana. Hadi wakati huo, jalia mtoto huyu akue na kubarikiwa na Mungu, awe na afya njema na nguvu, na awe mfano wa uwanawake katika siku zake zijazo. Nasi tutakupua sifa. Kwa maana tunamkabidhi huyu mtoto Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

<sup>11</sup> Nami namrudisha kwenu. Mungu awabariki. Bwana awabariki. Vema.

Kumbukumbu za thamani, jinsi zinavyodumu,  
Imetumwa rohoni mwangu kutoka mahali  
fulani;  
Yanapodumu, daima karibu nami,  
Matukio ya thamani, matakatifu  
yanafunuliwa.

<sup>12</sup> Jinsi tunavyomsifu Bwana wetu mpendwa kwa ajili ya watoto wote wadogo! Mnajua, linaonekana tu la kushangaza jinsi wakati mmoja tulivyokuwa wadogo namna hiyo. Na kuna kitu fulani kuhusu mtoto ambacho hakina ubinafsi, chenye kusamehe na chenye fadhili sana. Hata Bwana wetu aliwafananisha nao, na kusema, “Msipoongoka na kuwa kama mmoja wa hawa watoto,” rahisi sana.

<sup>13</sup> Ninamwona mtoto wangu Joseph, jinsi alivyo kwenye umri wa kuingia katika kila kitu, naye mama itambidi kumrekebisha. Naye ataondoa taa, ama chochote kile, ili tu asikie ikianguka sakafuni. Halafu basi ikitokea mama ampige, ama chochote kile, atapanda moja kwa moja mikononi mwake na kumkumbatia namna hiyo.

<sup>14</sup> Inatupasa kusamehewa, sisi kwa sisi, kama watoto hawa wadogo, tupate kuingia katika Ufalme.

<sup>15</sup> Sasa, tunamshukuru Mungu kwa ajili ya mtoto huyu mchanga, mtoto Mary Ella Branham. Na aishi, na kukua na kufanikiwa, na kuwa mtumishi wa Bwana. Na nyumba anayolelewa iwe ni nyumba ya Kikristo, kusudi aweze kukua katika maonyo ya Kristo.

<sup>16</sup> Na sasa tuna... (Asante, Dada Gertie.) Na sasa watoto wadogo wamechukua nafasi zao katika chumba cha madarasa ya shule ya Jumapili.

17 Naye mchungaji ame—amefanya matangazo ya mahali ibada zitakapokuwa leo, na kesho, kesho usiku. Alasiri ya leo, wataninii...nijuavyo mimi, hakuna ibada zilizo wazi, isipokuwa iwe ni baadhi ya misheni ndogo huko Louisville, tunazozifahamu, Ndugu yetu Durban na wengi wao. Nafikiri wana ibada ya Jumapili alasiri.

18 Nina simu nyingi. Watu wengi wako nyuani, na kadhalika, kuombewa, ambao ni wagonjwa na wanateseka.

19 Ibada zangu zijazo zitakuwa Cleveland, Tennessee, kuanzia Ijumaa ijayo usiku, Ijumaa hadi Jumapili.

20 Kisha tunakuja moja kwa moja nyumbani, na kwenda South Bend, Indiana, na kwa siku mbili usiku huko pamoja na kuwekwa wakfu kwa lile hekalu; Ndugu R. E. S. Toms kutoka Saskatoon, Saskatchewan.

21 Halafu basi, kutoka huko, tutaenda Sturgis, Michigan, kwa ibada ya siku mbili usiku huko Sturgis, Michigan.

22 Kisha twende huko Lima, Ohio, kwa Wabaptisti, katika Ukumbi wa Ukumbusho huko—huko Lima, Ohio. Hiyo inanza Januari ishirini na tatu, hadi ishirini na saba.

23 Na halafu, kutoka hapo, tutaenda kwenye Pwani ya Magharibi basi, kwenye mikutano mikubwa huko California na Arizona. Mwe katika maombi kwa ajili yetu. Kesho...

24 Usiku wa leo, saa moja na nusu, kutakuwa na ibada za uinjilisti hapa maskanini, na kila mtu amealikwa.

25 Na kesho usiku, sina budi...Nitazungumza kwa niaba ya Ndugu Cauble, kwenye—kwenye ibada yake ya mkesho usiku wa manane. Nitakuwa...Nafasi yangu itaanza saa tatu, hadi yapata saa tatu na nusu.

26 Kisha nitarudi maskanini hapa, ambapo mkutano tayari utakuwa unaendelea, pamoja na wachungaji na wahudumu wageni watakaokuwa hapa, ili kuwa na nafasi katika ibada ya kesho usiku. Ikiwa nyote mnapenda kusikia wachungaji wakizungumza na kuelezea njia zao za kuwaambia jinsi ya kuanza mwaka mpya, na cha kufanya, mbona, kutoka kwa mtazamo wa Kimaandiko, mbona, hakikisha utakuwa hapa kesho usiku. Ibada zinaanza saa moja na nusu, kama kawaida, saa moja na nusu. Na zitaendelea hadi usiku wa manane, Jumapili usiku, na kisha...ama, Jumatatu usiku, hasa. Halafu, baada ya saa tatu, baada ya kumalizana na Ndugu Cauble, nitarudi moja kwa moja hapa maskanini, kuanza, na pengine, labda, nimalize yale mahubiri ninayotaka kuanza asubuhi ya leo. Au, mimi ni...kidogo hunichukua muda mrefu.

27 Mimi ni mwenda pole, mwajua, lakini napenda Lenyewe lifikie kwenye msingi ufaao. Kwa hiyo, hakuna haja ya kulitawanya tu popote pale. Nataka likae pale, na likue na kufanikiwa kwa ajili ya Bwana.

<sup>28</sup> Sasa, kuna m—mhudumu hapa asubuhi ya leo, mhudumu kijana anayepaswa kuwa, nadhani, kwenye Moteli ya Bel Air. Ninapaswa kumwona ifikapo saa nane hadi saa tisa, alasiri ya leo. Na, au, yuko humu, bado? Kwa kuwa, nasahau jina la huyo ndugu. Anatoka huko Tennessee. Aliponywa mgongo uliovonjika, katika mkutano wangu, kisha akaingia katika huduma. Ndugu huyu, *hapo*. Vema. Hilo ni sawa. Hiyo ni. . . Hiyo ni kuanzia. . . Ilikuwa saa nane hadi saa tisa, sivyo? Mimi. . . [Ndugu huyo anasema, “Saa tisa.”—Mh.] Saa tisa; saa tisa hadi saa kumi. Vema.

<sup>29</sup> Halafu kuna mhudumu mwingine, sijui kama yuko hapa bado au la. Anatoka huko juu kabisa kaskazini mwa British Columbia. Sikujua moja, nilipokuwa nikijaribu kufungia sufuria, juu ya farasi fulani, nadhani, ama kitu fulani; Nilikuwa na ndevu ndefu *hivi*, nilikuwa nimerudi kwenye ziara ya mawindoni; miaka kadhaa iliyopita. Mtu mmoja akaja na kusema, “Je, wewe si Ndugu Branham?”

<sup>30</sup> Nilikutana na msichana fulani dukani, akasema hakuwa amewahi kuona mwanam-. . . au—au hajapata kuuona huo mji, mji mkubwa. Nami nadhani alikuwa maili mia nne ama tano kutoka mjini, labda zaidi ya hizo, mamia ya maili kutoka kwenye barabara isiyosakafiwa, katika mji mdogo unaoitwa East Pines. Nafikiri kuna duka moja hapa. Huko nyuma kabisa, mume na mke hawa walikuja.

<sup>31</sup> Nao wako njiani wakienda Kuba. Sijui kama wako hapa asubuhi ya leo, naam, kutoka kaskazini mwa British Columbia? Papa *hapa*. Vema, nakutakia heri, ndugu. Tuna furaha kuwa nawe pamoja na mke wako, wamishenari, mkipitia hapa. Alinipigia simu, asubuhi ya leo, kutoka—kutoka Moteli ya Star. Bwana awabariki. Ninajua kwamba ndugu zetu wote watafurahi kuwasalimia kwa mikono yao. Na mtu ambaye, kwa picha, angeweza kunitambua nikiwa na ndevu hizo zote, ana utambuzi mzuri. Nzuri sana.

<sup>32</sup> Nao walikuwa hodari sana, huko juu sana ambako karibu hakuna watu, huko juu sana katika East Pines. Na itakuwa, itakuwa ni vigumu kusema ni watu wachache kiasi gani wamepitia nchi hiyo, lakini, hata hivyo, walikuwa huko juu kama wamishenari, wakijaribu kufanya jambo fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Hakika ninawathamini kwa moyo wangu wote. Najua ninyi nyote mngenda kuwapa mikono na kusikia habari za nchi hiyo kubwa ya kaskazini-magharibi. Na, sasa, basi ninii. . .

<sup>33</sup> Ninaamini mama ya Bibi Roberson bado ni mahututi. Sina budi kumwona alasiri ya leo, na mkumbuke kumwomba. Hiyo itakuwa. . . Na halafu, Bwana akipenda, nitarudi hapa tena saa moja na nusu usiku wa leo. Nafikiri akina McSpaddin wako kule

nyuma, kwa kuwa tunaenda kula nao chakula cha jioni karibu thenashara, na itupe muda wa kurejea.

<sup>34</sup> Na kisha tunataka kumtembelea Bibi Burns. Je, Ndugu Burns yuko ndani, asubuhi ya leo? Je, yuko hapa? Naam. Sikukuona, Ndugu Burns, ukiketi. Dada Burns ni mgonjwa sana, mahututi.

<sup>35</sup> Nami nilikuwa huko hivi majuzi jioni, kumwona, naye ni mahututi. Naye ni mtu shujaa. Nasi tunataka kila mmoja amshikilie Mungu daima, kwa sababu, tukilielezea kwa njia hii, namna hii, bila kujua ni nani angekuwa hapa; bali itachukua mwujiza wa Mungu kumrudisha Dada Burns kanisani tena. Hiyo ni kweli.

<sup>36</sup> Wakati, mume wake mpendwa ndio kwanza atoke hospitalini kule juu, kwenye Hospitali ya Askari Wastaafu, akiwa na kansa, amehukumiwa kufa, na Mungu akamponya. Naye huyu hapa, amerudi kanisani, na akiwa na afya njema sana tena kama vile ingalitarajiwa katika wakati wa namna hii. Na wakati Bwana alipomponya wengu kuu ulioongezeka, ukiwa na kansa ndani yake, jambo lile lile, miaka na miaka iliyopita.

<sup>37</sup> Nami nakumbuka wakati ule ule, wakati Ndugu Wood anayeketi pale. Nilikuwa kwenye likizo ndogo. Tulikuwa huko msituni, tukiwinda kuchakulo, ndipo Kitu fulani kikaniambia, “Nenda nyumbani.” Nikaenda nyumbani. Na sababu ya kulazimika kwenda Louisville, sitajua kamwe. Naye Ndugu Wood, aliyelelewa kote Louisville, akiendesha gari mtaa ambao sio, akizunguka, tena, na tena, akijaribu kunichukua. Naye Mungu alikuwa akinizuilia kwenye kona moja, nikimngojea Dada Burns aje aniambie. Na ilikuwa ni yeye, mwanamke huyo shujaa, ambaye alikuja akaniambia mumewe alikuwa anakufa pale hospitalini, wakati tulipoenda pale na kuomba.

<sup>38</sup> Naye akashuka, na kuipiga picha hiyo, ambapo Bwana alipigwa picha Yake, ile Nguzo ya Moto...Ninyi nyote mmeiona, nadhani. Akaiweka chini sakafuni. Naye akasema, “Mpendwa Mungu wa Mbinguni,” akasema, “nisaide kumtafuta Ndugu Branham mara moja. Sina budi kumwona.” Naye akasema, “Malaika wa Mungu, niongoze kwake.” Hicho ndicho kinachohitajika. Naye anasimama, kisha anaenda mjini, kulipa bili ya matumizi, ndipo akaongozwa kwa njia ya ajabu kwenye kona nyingine. Naye Mungu akanituma kutoka msituni, hadi Louisville, na kunishikilia kwenye hiyo kona nusu saa, nikimtazama Ndugu Wood akipiga kona mahali pasipo wakati wote kule juu, akijaribu kunichukua, alikuwa. Mnaona?

<sup>39</sup> Sasa, tunajua ya kwamba Mungu anajua mahali maskini binti Yake amelala kule, Naye anaweza kuwa anawatarajia ninyi muombe maombi ya imani. Tutafanya yote tuwezayo.

<sup>40</sup> Jambo lingine tunalotaka kusema asubuhi ya leo, sio tu na vichwa vilivyo inamishwa, bali mioyo, kwa mmoja wa watu waaminifu sana ambao mimi... mmoja wao, niliowahi kukutana nao maishani mwangu, ni Ndugu yetu Higginbotham. Nanii wake... Dada yetu mpendwa ameenda kuwa pamoja na Bwana Yesu. Askari shupavu wa Mungu; ni mara ngapi nimemwona akija madhabahuni! Shauku yake ilikuwa, daima, kuingia kwenye mstari huu wa maombi, ambapo Roho Mtakatifu angemwambia shida ilikuwa nini. Alitamani kufanya hivyo. Na ni mara ngapi amepitia hapa jukwaani, akijaribu kuona kama upambanuzi unge—ungekuja. Na katika mikutano mingine na sehemu mbalimbali amejaribu, lakini haungekuja, kwa namna fulani.

<sup>41</sup> Na halafu, majuma machache yaliyopita, nikiingia hospitalini kule chini, niliposikia alikuwa mgonjwa, na ilikuwa jioni sana. Ndipo nilipoingia hospitalini na kuketi kando yake, hapo Roho Mtakatifu akashuka; akarudi moja kwa moja maishani na kuleta kila kitu, na kukiweka hasa mahali shida ilipokuwa. Lakini, jambo la ajabu lilikuwa, Dada Higginbotham hata hakutamani kukaa hapa tena. Alitaka kuondoka. Kulikuwa na kitu Fulani kilichokuwa kikimwita. Aliitikia wito huo hivi majuzi kwenda kuwa pamoja na Mungu. Nami sikuzote nitakumbuka hilo. Naam. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>42</sup> Si ajabu unajisikia vibaya unapoingia mjini; umeikataa Injili. Hiyo ndiyo shida. Nao umeandikiwa maangamizi. Ile gharika ya '37 haitakuwa kitu, hadi haya yatakapokwisha. Lakini, naam, umeandikiwa maangamizi, kabisa. Na hiyo ndiyo sababu maandiko ya mkono yako ukutani.

<sup>43</sup> Na, sasa, ni vibaya sana. Na tunamiliki mali, hivi vitu vilivyo hapa, lakini nilisikia juzi kuwa baadhi ya ndugu zetu walipewa tiketi kwa ajili ya kugesha gari hata ukingoni mwa sehemu ya kanisa pale. Aibu sana! Nitakulipia tiketi hiyo ikiwa tu utanijulisha ilikuwa ni nini. Linatia huruma. Naam, bwana. Naam, sisi, hii, nafikiri kama... Nafikiri bado tunamiliki hiyo. Angalau, hatimiliki inasema hivyo. Livute moja kwa moja kwenye hii hapa, na labda hutapata tiketi hapo. Lakini nina furaha kwamba tunaelekea mahali ambapo hawapeani tiketi. Nanyi je? Hiyo ni kweli. Ajabu. Naam, kabisa. Sasa, mimi si...

<sup>44</sup> Nitajaribu tu kuzungumza kwa muda kidogo, asubuhi ya leo, kwa sababu nilishikwa sana na homa kichwani, nikasimama. Na—nami ninataka kuchukua somo kutoka katika Agano la Kale, na kufundisha tu kwa muda kidogo, Bwana akipenda. Na halafu labda, usiku wa leo, kama tukirudi, Bwana akipenda, tukirudi kwa wakati mzuri, wala si wachovu sana.

<sup>45</sup> Loo, ilitokea tu niliwazia, pia. Ndugu Kelly anayeketi hapa, na Dada Kelly, watakuja, moja kwa moja kwenye... Njoni haraka mwezavyo, baada ya chakula cha jioni, maana nimetoka

tu alasiri ya leo, nikiwa na mambo mengi sana, Ndugu Kelly. Ninakumbuka hivi majuzi usiku, kule juu, nilikuwa nikitoka kwenye simu wakati nyote mlipoingia. Vema. [Dada mmoja anasema, “Je, utakuja, Ndugu Branham?”—Mh.] Sasa, hiyo ni—hiyo ni sawa, dada.

<sup>46</sup> Sasa, basi, niombeeni, na muombe...maamuzi yangu, kwa Bwana, yatakuwa—yatakuwa kwa ajili Yake, vizuri sana niwezavyo.

<sup>47</sup> Sasa, tunataka kukifungua Kitabu cha kale, cha kale, cha mwisho...Kitabu cha kwanza, Mwanzo 35, nasi tungependa kusoma sehemu ndogo tu ya Maandiko hapa kutoka katika Kitabu cha Mwanzo. Nasi tunaomba kwamba Mungu ataongeza kwa wingi baraka Zake kama msingi wa jambo tunalotaka kufundisha.

<sup>48</sup> Basi ni wangapi wanaopenda shule ya Jumapili? Loo, hiyo ni...Ni wangapi wanajua mahali ilipoanzia kwa mara ya kwanza? Sioni mkono. Kidogo ni...Ni wangapi wanajua ilivyoitwa kwanza? Mke wangu yuko wapi? Anapaswa kujua hilo. Vema. Ilikuwa...

<sup>49</sup> [Ndugu Neville anasema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Naam? [“Misheni...Mmishenari mwingine hapa asubuhi ya leo.”] Mmishenari mwingine. Mungu akubariki. [“Ndugu Naber.”] Ati Ndugu nani? [“Ndugu Naber.”] Ndugu Naber, yuko wapi? Je, waweza kuinua mkono wako, Ndugu Naber? Mungu akubariki, ndugu. Huyu aliye pamoja nawe ni mke wako? Hilo ni sawa kabisa. Tuna furaha kuwa pamoja nawe na familia yako asubuhi ya leo. Unajua uko katika mapenzi ya Mungu. Unaona? Huna budi kuwa, unapokuwa mmishenari, unaona. Kwa sababu, maagizo ya jumla ni, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.”

<sup>50</sup> Mtu ambaye ni mmishenari! Sasa, si—sijali sana... *Mishenari* ni neno zuri sana, lakini nina neno bora zaidi kwake. Wewe ni mtume. Unaona? Hiyo ni kweli. Sasa, neno *mtume* linamaanisha nini? “Mtu ambaye ametumwa.” Neno *mishenari* linamaanisha nini? “Mtu ambaye ametumwa.” Ni kitu kile kile. Kwa hiyo, wamishenari, manabii, wainjilisti, waalimu, na wachungaji, hufanya Kanisa. Hiyo ni kweli? Mitume, manabii...wanaitwa. Kwa hiyo, maadamu wewe ni mmishenari, ama mtume, wewe ni mtu aliyetumwa na Mungu, kwenye misheni, nawe sikuzote uko sahihi. Mungu awabariki, ndilo o—ombi langu.

<sup>51</sup> Ndugu na Dada Foss wako njiani kwenda Kuba, hudumani. Wanatoka maeneo ya barafu kali ya kaskazini, hadi kwenye misitu ya tropiki ya kusini, kwa maana Injili hii haina budi kuhubiriwa ulimwenguni kote. Amina. Ni badiliko jinsi gani!

<sup>52</sup> Unatoka wapi, ndugu? [Ndugu huyo anasema, “Ninakwenda Israeli sasa, ndugu.”—Mh.] Anaenda Israeli.



53 Loo, ningependa . . . Namwona Mabel ameketi kule nyuma, ningemwita mke wangu na Mabel, wawaimbie:

Wanatoka Mashariki na Magharibi,  
Wanatoka nchi za mbali,  
Kufanya karamu pamoja na Mfalme, kula  
kama mgeni Wake;  
Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!  
Wakiutazama uso Wake mtakatifu,  
Unaometameta kwa nuru ya Kiungu;  
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,  
Watakaong'aa kama johari kwenye taji Yake.

54 Si itakuwa ajabu sana siku hiyo! Amina. Bwana akubariki, huko Israeli; na wewe, mahali unapokwenda; ndizo baraka zangu kwenu ndugu asubuhi ya leo. Amina.

55 Sasa, kabla hatujaifungua Biblia . . . Tunajua ya kwamba hili ni somo, naye Mungu ana muktadha ulioandikwa katikati ya mistari, unaona. Kwa hivyo, tunaweza tu kusoma hili somo na kumwacha Mungu atupe muktadha. Kwa hiyo na tuinamishe vichwa vyetu kidogo tu, kwa maombi.

56 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba uyachukue Maneno haya ambayo tutasoma sasa, na kuyamega moja kwa moja mioyoni mwetu. Na tujalie tuje kwa upole, utulivu, unyenyekevu, uchaji, katika Uwepo Wako. Na jalia Roho Mtakatifu achukue Neno la Mungu na kulisha kila moyo. Jumuisha wangu hapo, je utafanya hivyo, Bwana? Kwa maana ninaomba katika Jina la Kristo. Amina.

57 Vema, tutasoma kifungu kimoja tu ama viwili, hapa, kusudi tuweze kupata msingi kidogo tu. Mwanzo ndicho mlango wa mbegu, tunajua. Vema. Tutaanza na kifungu cha 15.

*Mtu mmoja akamkuta, . . . tazama, alikuwa akizunguka-zunguka katika nyika: yule mtu akamwuliza, akisema, Unatafuta nini?*

*Akasema, Nawatafuta ndugu zangu: tafadhali, uniambie . . . wanakochunga mifugo yao.*

*Yule mtu—yule mtu akasema, Wametoka huku; kwa maana niliwasikia wakisema, Twendeni Dothani. Basi Yusufu akawafuata ndugu zake, akawakuta huko Dothani.*

*Ndipo walipomwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, kwa hiyo . . . ili wamwue.*

*Wakasemezana wao kwa wao, Tazama, yule bwana ndoto anakuja.*

58 Bwana na ajalie baraka Zake kwa Neno Lake. Sasa, Mwanzo sikuzote, kwangu mimi . . .

<sup>59</sup> Je, niliwaambia huo ulikuwa ni mlango gani? Ni Mwanzo. Ninaamini, kama niliona, Mwanzo 37, na kuanzia kifungu cha 15, nanyi mnaoliandika. Sasa sisi. . . Naamini nilisema 35, muda mfupi uliopita. Nilishika kurasa mbili pamoja. Ku—kunradhi. Maskini Biblia hii ya kale ya Scofield, na kidogo ni vigumu kwangu kusoma, kwa sababu nimepita arobaini, mnajua. Na ninii yangu. . .

<sup>60</sup> Wananiambia ninapaswa kuwa na miwani ya kusomea. Nilikwenda na kuchunguzwa macho yangu, nilipofikia ambapo ilinibidi kuendelea kuisukuma Biblia yangu mbali na mimi. Naye daktari ananiambia mkono wangu hautakuwa mrefu kutosha, baada ya kitambo kidogo, kuirudisha. Nami sina budi. . . Akasema ninahitaji miwani ya kusomea. Nikayachunguza macho yangu, nayo yalionekana makamilifu, kumi-kumi. Lakini ningeweza kuona unywele ukiwa sakafuni, mahali fulani pale, kwa urahisi tu. Lakini nikiiweka karibu nami. . . Akasema, “Utakapofikia. . .” Kasema, “Ni nini hufanya nywele zako ziwe za kijivu?”

Nikasema, “Sijui mimi.”

<sup>61</sup> Akasema, “Ni uzee.” Ha-ha-ha! Akasema, “Hiyo ndiyo shida ya macho ya mtu unapopita miaka arobaini. Wewe, kwa kweli, mboni zako za macho zinakuwa bapa. Nawe huna budi ku—kuvumilia hayo, hivyo tu.” Nami ninaendelea tu kuliahirisha. Na, vema, sina wakati wa kwenda, lakini ni—nitaenda siku moja, na kupima kitu cha ku—kusomea, nitakapoanza kufundisha zaidi. Lakini sasa ninasoma tu fungu la maneno na kuendelea. Na hii ni. . . Nilipata Biblia hii miaka mingi iliyopita, nayo ina, ina chapa ndogo sana.

<sup>62</sup> Sasa, katika Mwanzo, *Mwanzo* maana yake ni “chanzo,” mlango wa mbegu. Pia kumbukeni, ya kwamba, kila kitu kilichopo siku hizi, kwa kweli kilianzia katika Mwanzo. Ilikuwa ndio mwanzo wa mambo yote. Ilikuwa ni mwanzo wa—wa wokovu. Ilikuwa mwanzo wa dhambi. Ilikuwa mwanzo wa dini zote potovu. Ilikuwa mwanzo wa Kanisa la kweli. Ilikuwa mwanzo wa kanisa la uwongo. Ilikuwa mwanzo wa haki. Ilikuwa mwanzo wa udanganyifu. Ilikuwa ni mwanzo wa vitu vyote, vilianza katika Mwanzo.

<sup>63</sup> Laiti tungalikuwa na yapata miezi mitatu juu ya hili, kukaa moja kwa moja kwenye somo hili moja, na kulichambua tu, tulifunge kwa Roho Mtakatifu, kwa kamba za Mungu, na kulifunganisha tu pamoja. Pia angalieni jinsi kila Neno linavyoingiana moja kwa moja na hayo Maneno mengine. Jambo zuri sana!

<sup>64</sup> Neno la Mungu linatia moyo sana! Haidhuru ni wakati gani, kipindi kipi, kila mtu aliyewahi kusoma Andiko hili, kupitia kwa. . . Imeandikwa sasa kwa mamia mengi ya miaka, naam, karibu sana na elfu tatu, zaidi. Na kila mtu aliyewahi kusoma

Andiko hili, kwenye kila wakati, ametiwa moyo nalo, unaona, kila kifungu cha Maandiko. Hakuna kitu kingine kinachoweza kamwe kupachukua mahali Pake.

<sup>65</sup> Maandiko yaliyoandikwa huko nyuma katika siku nyingine, yanaposomwa kwa ajili ya wakati huo na kwa kusudi lake, yametosha. Ninaweza kukuandikia barua, na kusema, “Ndugu yangu mpendwa, leo nimekuwa mahali fulani na kufanya hivi na hivi, wakati fulani.” Hiyo imeelekezwa kwako moja kwa moja, na hiyo imetosha. Labda kwa ushahidi wa mahakama au chochote kile, ingeweza kuwasilishwa kwa ajili ya ushahidi dhidi yangu au kwa ajili yangu, kunithibitisha jambo fulani, au kuthibitisha jambo dhidi yangu, lakini haungekuwa ni ujumbe wa moja kwa moja jinsi ungalikuwa wakati umetolewa kwako.

<sup>66</sup> Lakini sivyo ilivyo Biblia. Imetolewa kwa jamii ya bianadamu, na kwa nyakati zote na kwa vizazi vyote, kwa sababu ni Neno la Mungu lililoandikwa. Mnaona? Maneno Yake hayawezi kushindwa kamwe. Hayatakufa kamwe, na maadamu kuna Umilele, daima na milele, haya bado yatakuwa na maana ile ile, kwa sababu yamekwisha kutoka katika midomo ya Mungu. Mnaona? Hayawezi kushindwa! Wazia tu jambo hilo, jinsi Neno la Mungu lilivyo la Milele. Ni Uzima.

<sup>67</sup> Sasa, neno ni nini? Neno ni wazo ambalo limetamkwa. Naye Mungu anapowazia jambo lolote, ni wazo tu. Lakini mara linapotamkwa, haliwezi kamwe kubadilishwa wala kugeuzwa. Halina budi kudumu milele.

<sup>68</sup> Maana, neno lako ni sawa tu na ulivyo wewe. Neno la Mungu ni sawa tu na alivyo Yeye. Neno lako ni sehemu yako. Ahadi yako ni sawa tu na unavyoweza kuwa. Nayo ahadi ya Mungu ni sawa tu na anavyoweza kuwa.

<sup>69</sup> Sasa, kwa kuwa u mwanadamu, unaweza kutoa ahadi na ikakubidi kuivunja, kwa sababu wewe ni mwanadamu tu. Mimi ni mwanadamu tu. Lakini, Mungu, kwa kuwa si mwanadamu, wala hana kikomo, na mwenye nguvu zote, anayeenea kila mahali, Yeye hutoa tamshi, Naye anajua mwisho tangu mwanzo, Naye anaweza kulitimiza.

<sup>70</sup> Ibrahimu aliviita vitu visivyokuwapo, kana kwamba vilikuwako, kwa maana alishawishika kabisa ya kwamba, yale Mungu aliyoahidi, Mungu aliweza kuyatimiza, maana Yeye asingalitoa ahadi isipokuwa alijua yatakayotukia.

<sup>71</sup> Mnaona jinsi tunavyoweza kutulia juu ya Neno Lake basi? Haidhuru dhoruba inavuma kwa nguvu jinsi gani, ni kitu gani kinacholipinga, tulia kwa uchaji juu ya Neno. Mungu alisema Hilo, Ambaye ameona ng'ambo ya hiyo dhoruba. Unaona? Kwa hivyo, ikiwa wewe ni mgonjwa, itie tu nanga nafsi yako katika Mahali pa Raha. Ikiwa unafadhaika na kuhuzunika, kumbuka, Yeye alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Na Yeye ni . . . Alisema, “Mambo yote hufanya kazi

kwa wema kwa wale wanaompenda Bwana,” kwa hiyo kaa hapo tu.

<sup>72</sup> Mtu mmoja aliandika, mshairi aliandika, “Nanga yangu inashikilia ndani ya pazia.” Pazia ni nini? Ni kitu kinachofunga huku kutoka Huko. Nayo nanga iko ndani ya pazia. Huoni jinsi itakavyokuwa, lakini unajua ya kwamba kuna kitu fulani ambacho kimekushikilia, ambacho kimeshikilia Huko juu.

<sup>73</sup> Basi bahari inapovuma na kuchafuka, je, uliwahi... Nadhani labda baadhi yenu hamjapata fursa ya kuona meli imetia nanga. Loo, jamani! Nimezipanda wakati wanapotupa nanga ya bahari namna *hiyo*, mpaka maskini chombo hicho kisingeweza hata kwenda juu ya wi—wimbi. Kingepitia ndani ya wimbi. Lakini maadamu nanga ilishikilia, hiyo ndiyo tu inayoleta tofauti yoyote.

<sup>74</sup> Kama tunapitia juu yake, chini yake, kando yake, au kupitia humo, haijalishi; nanga inashikilia. Ndivyo ilivyo wakati dhoruba za maisha zinapoanza kututikisa. Tunaweza kulazimika kupitia humo, tunaweza kulazimika kupitia juu, chini, kando, ila tu acha nanga ishikilie ndani ya pazia, kwa mambo yasiyoonekana. Hatujui iko wapi hasa, lakini inashikilia.

<sup>75</sup> Kama tu yule mvulana mdogo, mnajua, ambaye alikuwa na tiara. Mmeisikia hiyo methali ya kale, ile hadithi. Kasema, “Unajuaje una tiara kule nchani?”

Kasema, “Ningali ninaweza kuhisi ikivuta.”

<sup>76</sup> Kwa hiyo, ndivyo hivyo. Ikiwa tunaweza kuhisi ingali inavuta, Mungu akiishughulikia mioyo yetu, basi tunajua nanga yetu ingali inashikilia.

<sup>77</sup> Ninaamini ilikuwa ni Benjamin Franklin aliyeinasa radi kwa chupa, ambaye aliunganisha radi, umeme. Kitu fulani ndani yake kiliita, na kusema, “Kuna nguvu ndani ya hiyo. Nguvu hizo zingeweza kuunganishwa.” Na ikiwa zina nguvu hivyo, kuenea mitaani na kupasua mbao, kuipasua ardhi, zingeweza kufanya nini mara zikiunganishwa? Zitamulika, na kuwaka, na kuenea kote duniani. Basi Benjamin Franklin, naamini, akituta tiara yake, huku ufunguo umefungiwa nchani mwake, na chupa upande wa chini. Ndipo alipoipata, hakujua alichokuwa nacho, bali akaanza kupiga mayowe, “Nimeipata! Nimeipata!” Hakujua ilikuwa ni nini; hakujua atakachofanya nayo; ila alijua alikuwa na kitu fulani.

Basi ndivyo ilivyo kwa kila mtu ambaye ninii yake:

Matumaini hayajajengwa juu ya kitu chochote  
pungufu  
Ya Damu ya Yesu pamoja na haki;

Basi yote yaliyo karibu na nafsi yangu  
yakiondoka,  
Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na nanga  
yangu.

Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara,  
nasimama;  
Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao.

<sup>78</sup> Mara baada ya kuzaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu huchukua nafasi Yake moyoni. Baadhi ya vijana huenda wasiweze, ama vijana, ama wanaweza kuwa hawana elimu, haidhuru ikoje; hakuna anayeweza kulielezea, kwa hivyo usijisikie vibaya kwa sababu huna elimu. Usingeweza kulielezea. Bado hapajakuwapo na mtu angaliweza kulielezea, haidhuru ni mwerevu au ana akili jinsi gani. Ni siri ya Mungu Mwenyewe. Lakini wakati Neno hilo linapokuwa Hai moyoni mwako, nawe unaliona, unapiga mayowe, “Nimelipata!” Hujui utakayofanya nalo; hujui litavyokufanyia; ila unajua jambo fulani limetukia, nawe umelipata.

<sup>79</sup> Sasa, basi, juu ya Neno! Ni nzuri. Sasa tunakabiliwa asubuhi ya leo, na tunalo mbele yetu, kulizingatia, nionavyo mimi, mojawapo ya maandiko muhimu sana ya Agano la Kale. *Yusufu* (tutalizungumzia) *Akikutana Na Nduguze*. Kunaweza kuwa na njia mia moja mbalimbali ambazo Roho Mtakatifu ataingia katika hili na kulifunulia mioyo yetu na akili zetu. Kwa hiyo, tukiliwazia hili, wakati tukiwa hapa siku chache, huenda tukazungumza kidogo asubuhi ya leo, kwa sababu ya mkazo kooni, na labda tulichukue tena usiku wa leo kama mchungaji hana lolote moyoni mwake, na labda tuliendeleze na kulimalizia Jumatatu usiku, ikiwa Mungu atalijalia hivyo.

<sup>80</sup> Sasa, tunafahamu vyema sifa bainifu za Agano la Kale, jinsi ambavyo, “Mambo yote ya zamani za kale yalikuwa ni kivuli,” Waebrania 11, “kivuli cha mambo yatarajiwayo.” Jinsi hilo lilivyo zuri, jinsi Mungu anavyotangulia kuonyesha mambo!

<sup>81</sup> Basi tunapokihisi kivuli hiki, tuseme, tunajua ya kwamba kuna kitu baada ya hapa. Ninii. . . Mungu, katika uweza Wake, katika nia Yake kuu isiyo na kikomo, akiona jambo likikaribia kutukia, anaweza kulitolea onyo kimbele. Anaweza kufanya kila kitu kifanye kazi pamoja, hata hasira ya mwanadamu, ipate kumsifu Yeye, hata mtu anayekutendea maovu. Kama tutakavyoona, baada ya muda kidogo, Bwana akipenda, jinsi ambavyo ndugu yake Yusufu alivyomtendea maovu, Naye akageuka nyuma moja kwa moja, na kulichukua hilo na kulifanya limsifu. Kwa hivyo, hatuna lolote la kututia wasiwasi, hata kidogo.

<sup>82</sup> Jinsi ambavyo Mungu, kupitia kwa mvulana huyo, alikuwa akionyesha kimbele kuja kwa Bwana Yesu mara ya kwanza, na kuja Kwake Bwana Yesu mara ya pili, na akatekeleza yote katika

maisha ambayo hayakujua lolote kuhusu kile kilichokuwa kikiendelea. Amina. Je, hilo halikufanyii tu jambo fulani, kumwona maskini mtoto Yusufu? Mbona, hakujua kilichokuwa kikitendeka, kwa nini mambo haya yote yalipaswa kutokea. Bali yote yalikuwa ni Mungu, akitenda kazi, akitangulia kuonyesha, akionyesha kimbele mambo yajayo.

<sup>83</sup> Ndipo unaweza kuona Neno, jinsi unavyolichukua hapa na kulisoma katika Mwanzo, unalisoma katikati ya Kitabu, unalisoma mwishoni mwa Kitabu, na kila Neno linakubaliana na lingine moja kwa moja namna hiyo. Nayo yaliandikwa yakiachana kwa maelfu ya miaka, na mamia ya watu mbalimbali. Mnaona? Kwa hiyo, basi, mnaona yote ni Mungu. Mmoja bila kumjua mwenzake, ama kujua ni Kitabu gani kilichoandikwa, hakuna kitu juu Yake; kipindi kingine, wakati mwingine.

<sup>84</sup> Nasi tunaweza kuona, leo hii, ya kwamba Mungu anatenda sawasawa hasa na alivyotenda kule nyuma. Tunaelekea tu sasa hivi, tukiishia katika mwaka mpya, kutokana na kuonyeshwa kimbele cha Kale. Na jinsi ambavyo hapo mwanzo, jinsi ambavyo Mungu, alipoona dhambi ikichukua mamlaka yake juu ya dunia na juu ya watu, jinsi ambavyo ule mpango mkuu ulikuwa umepotoshwa; si kuharibiwa, si kuundwa upya, lakini kupotoshwa tu.

<sup>85</sup> Mnaona, Shetani hawezi kuumba. Anaweza tu kupotosha. Kila kitu unachokiona, ni kibaya, hiyo ni haki iliyopotoshwa. Unaona? Ukimwona maskini mpiga ramli huko nje mitaani, huyo ni manabii tu waliopotoka. Mnaona? Ukiona chochote ambacho ni kiovu, ukimwona mwanamume akiishi bila uaminifu kwa nadhiri zake kwa mkewe, hiyo ni haki iliyopotoshwa ikawa uovu. Vinginevyo, ukiwaona wanawake mtaani, wakitenda jinsi wanavyofanya na kuwa jinsi walivyo, hao ni wanawake waliopotoka.

<sup>86</sup> Nilipitia Louisville, hivi majuzi, mimi na mke wangu, nami nikaona ubao dirishani, tulipokuwa tukitoka kula, kwenye Barabara ya Tano. Nao ulisema, “Meza za mama wa heshima.”

<sup>87</sup> Nikasema, “Hawajawahi kupata mteja.” La, mama mwenye heshima asingeingia humo. Anapoingia mle, yeye si mama mwenye heshima tena. Unaona? Kwa hiyo, hawakuwahi kupata mteja, chini ya ubao huo. Mama wa heshima hawaendi mahali hapo. Lakini, mnaona, wanaoingia mle, ni wanawake waliopotoka. Mnaona? Vema.

Sasa, Mungu, kufanya vitu vyote vimsifu!

<sup>88</sup> Tunasherehekea Krismasi, kuzaliwa kwa Bwana Yesu. Ambayo, siyo siku ya kuzaliwa Kwake hasa. Siku ya kuzaliwa Kwake ilikuwa Aprili. Maana, ni baridi huko Uyahudi, ama baridi zaidi mnamo Desemba, kuliko ilivyo hapa. Kwa hiyo, tunatambua hilo. Mliiona ile picha hivi majuzi, vile vifarua huko

juu kwenye theluji, na kadhalika namna hiyo, huko Uyahudi. Je, ungeweza kuwazia wachungaji wakikaa mlimani katika hali kama hiyo ya hewa? Lakini, hiyo siyo ile siku. Lakini hiyo, hiyo siku, haimaanishi mengi sana, ni—ni mtazamo tulio nao kwa siku hiyo iliyotengwa.

<sup>89</sup> Sasa angalieni. Mara tu Mungu alipouona ule uzao wa mwanamke, na jinsi walivyoeleweka vibaya huko na haki ilikuwa imepotoshwa, Mungu alitoa ahadi kwamba kupitia mwanamke huyo angekuja Uzao uliobarikiwa. Mnalipata? Kungekuwa na Uzao.

<sup>90</sup> Na mara tu Shetani aliposikia hayo, ambaye alikuwa amesimama pale, mara tu aliposikia hilo, aliingilia kuiharibu huo Uzao. Ndipo akajaribu kuiharibu katika Yusufu. Akajaribu kote katika wakati. Naye angali anaupinga Uzao huo uliobarikiwa. Amina.

<sup>91</sup> Nataka mvae kofia zenu za kutafakari kwa kina, kwa dakika moja tu sasa. Basi, vaa chapeo ya wokovu, na usikilize kwa makini sasa. Hili hapa jambo muhimu sana. Na unaweza kukosa kukubaliana nalo; ni sawa. Lakini, je, mliona, mara tu. . .

<sup>92</sup> Tayari kulikuwa na mi—mimba, kwa maana Hawa alikuwa tayari ameishi vibaya na alikuwa ametenda dhambi. Hiyo ilitoka wapi? Hiyo iko katika Mwanzo. Watu siku hizi wanajaribu kutafuta kiungo kinachokosekana kati ya mnyama na mwanadamu. Huu ni ufunuo. Biblia ilisema, kwamba, “Nyoka akamdanganya mwanamke.”

<sup>93</sup> Siku hizi, mwanadamu anaweza kuleta uhai wa wanyama, na mnyama aliye karibu zaidi na mwanadamu ni sokwe. Wanaweza kumfanya avute kiko, apande baiskeli, avae kofia, aainamshie upande. Hiyo ni kama tu “guu” na “hoo” kwa farasi. Ni sauti. Yeye hana nafsi. Hawezi kufikiria. Anaweza tu kwenda kwa sauti. Hana nafsi. Halafu wana kiungo kilichokosekana, mumu humu katikati, ambacho kamwe hawajaweza kukipata. Na kwa miaka elfu sita wamejaribu kupata miong’ono mmoja kutoka kwa sokwe, wala hawawezi kuupata. Kamwe hawataupata. Lakini, tunajua kwamba sisi ni uhai wa mnyama. Sisi ni uhai wa mimea, kutoka ardhini.

<sup>94</sup> Kama nilivyokuwa nikisema hivi majuzi, kwenye mazishi ya dada yetu mpendwa. Sisi ni lundo la elementi kumi na sita za dunia, za nurulimwengu, na petroli, na vitu vilivyowekwa pamoja. Tulikuwa hapa Mungu aliponena na kusema, “Na iwe.” Miili yetu ilikuwa. Lakini, kitu Fulani, Akili kuu ikatutengeneza tukawa jinsi tulivyo sasa. Akatuumba tukiwa na viganja vya mikono na mikono, na kadhalika, sio kutuungamiza, bali tupate kuishi milele. Dhambi ikasababisha uharibifu. Na Yeye aliyetuumba, bila sisi kuwa na fu—fununu yoyote ya kuwa hapa, Yeye aliyetuumba na kuleta vitu hivi pamoja na kutufanya jinsi tulivyo sasa; si anaweza hata na zaidi, kwa kutupa

uhuru wa kujichagulia tupate kulikubali, na kwa Neno lile lile lililotuumba, akatuhidi ya kwamba angetufufua tena. Ni zaidi sana vipi petroli hizi zote zitakavyokusanyika pamoja, na atomi, na kadhalika, katika . . . kwa Neno la Mungu!

<sup>95</sup> Sasa, hapo mwanzo, wakati Mungu aliponena, naye Shetani alikuwa amesimama pale naye akasikia.

<sup>96</sup> Nao watu wanajaribu kutafuta kiungo hiki kisichopatikana. Nitawaambia, kwa ufunuo, mkitaka kuupokea. Mtu huyo asiyeapatikana, kati ya mnyama na mwanadamu, ni nyoka, kabla hajanyang'anywa miguu yake. Biblia ilisema, "Alikuwa mwerevu kuliko hayawani wote," sio mtambaaaji, "wote wa mwituni." Yeye ndiye aliyemdanganya mwanamke, kwa urembo wake, naye akapata mimba. Na sasa, kwa kufanya hivyo, na kuona dhambi ilikuwa inakuja, Mungu aliweka laana kubwa sana juu yake mpaka sayansi haitapata uhusiano wowote kati ya nyoka huyu, kama anavyojulikana siku hizi, na binadamu. Lakini huyo hapo mtu wako aliyeanguka, aliyeshushwa hadhi, katikati, aliyeunganisha maisha ya hao wanyama pamoja. Haya basi.

<sup>97</sup> "Mungu amelificha wenye hekima na busara, lakini atawafunulia watoto wachanga watakojifunza." Mnaona?

<sup>98</sup> Huyo hapo mtu wako aliyeanguka, yule nyoka. Aliletwa kutoka mbali. . .mwerevu kuliko wote, mkuu zaidi, mrembo zaidi, aliyefanana zaidi na mwanadamu. Halafu basi kwa sababu ya uovu huu aliofanya na Hawa, akamshusha akawa mnyama mtambaaaji, "Kwenda kwa tumbo lake, siku zote za maisha yake, na mavumbi yanapaswa kuwa chakula chake." Hapo ndipo sayansi inapoweza kufikia pale, nao mti wao unaangukwa.

<sup>99</sup> Angalieni, sasa, mara mwanamke alipoona ya kwamba yeye. . .ya. . .Sasa, alidanganywa kabisa. Hakuileta dhambi. Alidanganywa. Alidhani ilikuwa ni sawa. Lakini, "Adamu hakudanganywa," ilisema Biblia. Alijua ilikuwa ni makosa, naye mwanamke akamfanya afanye jambo lile lile ambalo yule mnyama alikuwa amefanya.

<sup>100</sup> Naye akamzaa mwanawe wa kwanza, ambaye, tabia zote bainifu za ibilisi zilikuwa ndani ya mvulana huyo. Alikuwa mwuaji. Alikuwa na wivu. Ingewezaje kutoka kwenye mkondo huo safi wa Mungu? Ilibidi itoke kwa yule mwovu. Na mara alipofanya hivi, basi yeye, ibilisi, akatumia kifa chake.

<sup>101</sup> Akamzaa mwanawe wa pili, ambaye alifanana na Adamu, na hapo ndani alikuwamo Habili. Na, upesi sana, ibilisi akajaribu kuuangamiza huo uzao wa haki. Naye akageuka na kumwua Habili, kwanza kabisa; ambalo ni mfano wa Yuda na Yesu. Akamuulia madhabahuni; ambapo, Yesu, Yuda alimwua—alimwulia Yesu, akamsaliti kwa vipande thelathini vya fedha na kumuua. Vema.



<sup>102</sup> Lakini, angalieni. Alipofanya hivyo, ndipo Mungu, mfano wa Kristo, kufa na kufufuka pia, Yeye akamwinua Sethi kupachukua mahali pake. Mnaona? Naye ibilisi akamwandama Sethi.

<sup>103</sup> Sasa tazama. Kwenye, kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, kulikuwa na ukoo mrefu wa watu walioshuka kupitia wana wa Kaini, kutoka nchi ya Nodi, nao walikuwa wanasayansi, werevu, wenye akili, watu wa ajabu. Wao hata walifua vyuma. Walijenga nyumba. Walikuwa ustaarabu wa ajabu. Biblia inaendelea na kusema jinsi walivyotumia shaba, jinsi walivyotumia chuma.

Lakini, kundi hili lingine lilikuwa ni wazururaji.

<sup>104</sup> Lakini, makundi yote mawili yalikuwa ya kidini. Kaini alikuwa mtu wa kidini. Habili alikuwa mtu wa kidini. Naye Mungu akachora mstari, ni nani aliyekuwa sahihi. Kaini alikuwa wa kidini tu kama Habili. Wote wawili walijenga madhabahu. Wote wawili walimwamini Mungu. Wote wawili walimwabudu Mungu. Wote wawili walileta zawadi.

<sup>105</sup> Sasa ziangalieni hizo mbegu mbili. Mmoja, anapiga vita; yule mwovu akijaribu kuuangamiza Uzao wa haki. Naye akajaribu kumwangamiza Habili; akamwangamiza, lakini Mungu akamwinua Sethi apate kupachukua mahali pake. Alidhani alimpata Yesu papo hapo. Angalia kote katika wakati, kila mahali. Yeye, kila mahali alipokuja, aliuzinga Uzao huo. Alipomwua mmoja, ama mwingine, alidhanika amempata Huyo. Na, hatimaye, a—akamfuatilia Yohana Mbatizaji, hatimaye akamkata kichwa. Alidhani alimpata basi, bali aligundua kuwa alikuwa hapa katika Yesu. Aliwaua watoto wote. Pia, Musa; alijaribu kumwua Musa. Alijaribu kila njia aliyoweza kuuangamiza Uzao huo, ndipo alipomwua Kristo pale Kalvari; lakini Mungu alimfufua tena, siku ya tatu, kisha akamtuma Roho Mtakatifu tena kuwaita wana na binti kwa Mungu. Na mbegu iyo hiyo ovu ya kidini, inautesa Uzao huo wenye haki hata wa leo. Mnaliona? Wanajaribu kuliharibu hilo Tawi la haki la Mungu.

<sup>106</sup> Sasa, pande zote mbili, kama ukiangalia, ilianza katika Mwanzo, wa kidini pande zote mbili. Mmoja wao, wa kimadhehebu, mwenye kujivuna. Na huyo mwingine, mnyenyekevu, akitembea katika Roho, kwa ufunuo.

<sup>107</sup> Habili angewezaje kujua ya kwamba ilikuwa ni mwana-kondoo badala ya matunda ya kondeni? Kwa sababu ilifunuliwa kwake, kwa ufunuo wa Kiungu.

<sup>108</sup> Yesu alisema vivyo hivyo, hapo Petro alipomkiri kuwa Mwana wa Mungu. Alisema, “Mwili na damu havikukufunulia hili, ila Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Juu ya mwamba huu...” Ule mwamba, si Petro, si Yesu, bali juu ya ufunuo wa Kiungu. “Nitalijenga Kanisa Langu, na malango

ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Mnalipata? Ni ufunuo wa Kiungu.

<sup>109</sup> Sasa tazama. Kila juhudi, ya wakati, pale, walikutana uso kwa uso na kupigana. Angalieni wakati Moabu walipokuwa juu ya kilima, nao Israeli walikuwa bondeni. Nao Israeli wakiomba tu kama ndugu, mwungwana, kupitia nchini mwao, wakienda kwenye nchi ya ahadi ambayo Mungu alikuwa amewaahidi; waliomba tu uamsho mdogo kanisani mwao, tuseme. Kupitia tu humo nchini, nao wakaahidi hata wangelipia nyasi ambazo ng’ombe walikula. Nao wangepitia katika njia kuu ya mfalme, na mambo ambayo wangepitika walipokuwa wakipita humo nchini, na wangelipia. Lakini, wivu . . .

<sup>110</sup> Sasa, Moabu, nchi ya Moabu haikuwa ya kikafiri. Walikuwa wanamwamini Mungu yeye yule ambaye Israeli walimwamini, kwa kuwa walikuwa wana wa binti za Lutu; Binti ya Lutu ambaye alishika mimba wakati Lutu alikuwa amelewa, ya baba yake mwenyewe. Nao wakavuka, na wao . . . Hapo ndipo Wamoabu hawa walipotokea.

<sup>111</sup> Basi nabii wao alipojitokeza, mwalimu wao, mwenye kichaa cha pesa, na kujenga madhabahu, madhabahu saba, idadi iyo hiyo hasa ya madhabahu ilihitajika hapa chini. Huyu hapa Moabu ameketi hapa, ile nchi kuu nzuri ya kimadhehebu, yote ikiwa salama salimini.

<sup>112</sup> Na hawa hapa Israeli, maskini mtakatifu anayejibingirisha wakirandaranda katika mahema, mahali mahali. Mnasema, Ati “Mtakatifu anayejibingirisha”? Hakika ndivyo walivyokuwa, kama wa—wao ni kile wanachoita, siku hizi, mtakatifu anayejibingirisha.

<sup>113</sup> Walipovuka Bahari ya Shamu, naye Mungu akafanya muujiza mbele zao, Miriamu alinyakua tari na kuanza kupiga tari, na kukimbia ukingoni, akipiga mayowe na kuruka-ruka, na kucheza katika Roho. Huku mabinti wa Israeli wakimfuata, wakiruka-ruka, wakipiga mayowe, wakicheza katika Roho. Naye Musa akasimama ameinua mikono yake juu, labda akiimba kwa lugha ambayo hakuna mtu aliyewahi kuisikia hapo kabla, wimbo ambao hakuna mtu angeweza kuelewa. Alimwimbia Bwana, katika Roho. Kama hao si watakatifu mamboleo wanaojibingirisha, sijui niwatafute wapi. Walikuwa na ishara na maajabu.

<sup>114</sup> Sasa, kama Mungu anaheshimu tu mambo ya kimsingi, angalieni hapa. Moabu, tukinena Kimaandiko, walikuwa wa kimsingi tu kadiri Israeli walivyokuwa. Alikuwa na kila kitu ambacho Israeli walikuwa nacho. Alikuwa na madhabahu saba. Hayo ndiyo Mungu aliyohitaji; Israeli walikuwa na madhabahu saba. Alikuwa na dhabihu saba safi. Israeli walikuwa na dhabihu saba safi. Hao hapo Kaini na Habili, tena. Mnaona? Vema. Alitoa mafahali saba. Alitoa mafahali saba. Akatoa

kondoo waume saba, wakinena kwamba... akiamini kwamba Kristo atakuja. Alitoa kondoo dume saba, kitu kile kile. Wa kimsingi tu iwezavyo kuwa!

<sup>115</sup> Kaini alijenga madhabahu; Habili akajenga madhabahu. Kaini alitoa dhabihu; Habili akatoa dhabihu. Habili aliabudu; Kaini akaabudu. Lakini, Mungu alithibitisha, alithibitisha ya kwamba Habili alikuwa ndiye chaguo Lake.

<sup>116</sup> Mungu alithibitisha hapa ya kwamba Israeli walikuwa ndio chaguo Lake, kwa maana Israeli walikuwa na nguvu za kimbinguni kambini mwao. Ingawa, pamoja na makosa yao yote, walikuwa na Nguzo ya Moto ikiwafuata. Walikuwa na upatanisho kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, na wakafanya uponyaji wa Kiungu; nyoka. Walikuwa na mwamba uliopigwa. Walikuwa na ishara na maajabu kambini.

<sup>117</sup> Yohana alipokuja, alikuwa wa kimbinguni. Yesu alipokuja, ilikuwa ni ya kimbinguni. Naye adui, upande wa kimsingi, daima aliwatesa wa kimbinguni.

<sup>118</sup> Mnaona anachojaribu kufanya siku hizi? Kitu kile kile, "Kufutilia mbali uponyaji wa Kiungu! Kuwafutilia mbali watu hawa! Hawafai kitu!" Waheshimiwa, watu mashuhuri! "Wafutilie mbali!" Ndugu, si kitu ila mزابibu huo, unaopinda kupitia Mwanzo, ukiingia katika Ufunuo.

<sup>119</sup> Ninawaunga mkono watakatifu wanaojibingirisha!...?... Acha iwe chochote... Sijawahi kumwona mtakatifu anayejibingirisha. Hilo ni jina ambalo ibilisi alilibandika Kanisa la Mungu, wakati si lao. Wao si watakatifu wanaojibingirisha. Wao ni wana na binti za Mungu, walioeleweka vibaya na ulimwengu.

<sup>120</sup> Sasa, Yusufu alizaliwa na baba yake, na alipendwa na baba yake, na kuchukiwa na nduguze. Sasa angalieni, picha kamili ya Bwana Yesu. Ninawatakeni muone jinsi maisha Yake yalivyofananishwa tu, katika Agano la Kale, kila kitu kilifananishwa sasa. Angalieni huko nyuma muone ile picha; hicho hapo kivuli, nawe unaona cha halisi ni nini. Sasa angalieni, Yusufu, akiwa mfano wa Kristo, mfano wa Kanisa, mfano wa Roho Mtakatifu. Mfano... Alikuwa mfalme wa ufanisi, kama tu alivyo Kristo, kama tu Kanisa siku hizi.

<sup>121</sup> Angalieni, tena, ya kwamba, alipozaliwa, baba yake alimpenda na akamshonea kanzu ya rangi nyingi. Sasa, kuna rangi saba tu kamilifu katika rangi zote. Nyingine zote zinafanyizwa kutokana na rangi hizi. Nayo hiyo kanzu labda ilikuwa na rangi ndani yake, ya rangi saba mbalimbali, milia ya rangi, ndani ya kanzu ambayo baba alimshonea. Mkiangalia, labda Yakobo hakuelewa hilo wakati huo, lakini hiyo iliashiria "Aliyehidiwa." Mungu alipompa Nuhu ile ishara ya upinde wa mvua, zile rangi saba, ilikuwa ni ahadi, ama Ya Agano. Mungu

alikuwa amefanya agano kwamba hatauangamiza ulimwengu tena kwa maji.

<sup>122</sup> Nalo agano la Mungu pia liliendelezwa kupitia kwa Yakobo, hadi kwa Yusufu. Ibrahimu alikuwa uteuzi, naye Isaka alikuwa kuhesabiwa haki, naye Israeli alikuwa neema, na Yusufu alikuwa ukamilifu. Huyu ndiye pekee aliyekuwa na zile rangi.

<sup>123</sup> Tunamwona Yesu ameketi juu ya Kiti cha Enzi, akiwa na zile rangi, upinde wa mvua umemzunguka, katika Ufunuo 1. Ilikuwa ni agano la Mungu pamoja na watu. Kristo... Hili hapa. Loo, jinsi ninavyotaka mlione! Kristo ni agano la Mungu pamoja na watu Wake. Si madhehebu; lakini Kristo ndiye agano la Mungu.

<sup>124</sup> Kama vile Yusufu alivyochukiwa, ndivyo Kristo anavyochukiwa siku hizi. Hawataki kusema wanamchukia Kristo, lakini matendo yao yanathibitisha kile wanachofanya. Wanapinga kila hatua Yake; wanazungumza juu ya matendo Yake, kazi Zake, matendo Yake ya ajabu. Vema, hakika, tuna Shetani kambini, pia, akipiga vita. Hakika. Na wataelekeza kwenye maneno ya Shetani. Lakini, sijali Shetani anafanya nini ku—kujaribu kutatanisha. Neno la Mungu linasimama kikamilifu, nayo ahadi Yake ni kamilifu. Sitataka kamwe kuungana na kundi hilo.

<sup>125</sup> Angalia, Huyu hapo, lile Agano. “Kristo alionekana kama jiwe la yaspi na akiki,” katika Ufunuo. Hilo lilikuwa ni jiwe la kifuani... jiwe la kuzaliwa, hasa, kutoka kwa Rubeni hadi Benyamini. Huo ulikuwa ni ukisi wa akiki na yaspi, yalipoakisi pamoja chini ya Nuru ya Mungu, akafanya agano kumzunguka Kristo, ule upinde wa mvua. Basi inanena juu ya nini? Rubeni, kifungua mimba; Benyamini, kitinda mimba! Kutoka wa kwanza hadi wa mwisho, “Yeye ndiye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina, Mzao wa Daudi. Yeye ndiye Nyota ya Asubuhi. Yeye ni kuanzia A hadi Z; Alfa, Omega; Ukisi wa Mungu tangu mwanzo wa wakati hadi mwisho wa wakati. Huyu hapo, agano la Mungu pamoja na watu Wake.

<sup>126</sup> Na mambo haya mengine yote, Yusufu, Daudi, manabii wote, walikuwa tu ni ukisi. Amina. Ukiakisi, kutoka kwa Uzao wa kweli tangu bustani ya Edeni, mpaka wakati atakapokuja mara ya pili, katika Utukufu, kuwapokea watu Wake na Kanisa Lake. Hilo hapo, lapendeza ukilitazama.

<sup>127</sup> Yusufu, ndugu zake walikuwa na kiburi kwake. “Walimchukia, bila sababu,” kwa sababu alivuviwa kimbinguni. Mnalipata? Kaini alimchukia Habili, bila sababu, kwa sababu ya kuongozwa kimbinguni. Moabu waliwachukia Israeli, bila sababu, kwa sababu walikuwa na uponyaji wa Kiungu, ishara, maajabu, na miujiza. Walimchukia, bila sababu, wala wasingemruhusu apite... .

<sup>128</sup> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... kumchukua mke wa ndugu yako. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

<sup>129</sup> Sasa, rafiki zangu wapendwa, nataka kuwakumbusha jambo fulani, nami nataka mliweke chini ya ubavu wa tano upande wa kushoto, katika hema la chumba hicho kiitwacho moyo.

<sup>130</sup> Hakuna, katika wakati wowote au kipindi chochote, ambao Mungu aliwahi kumvuvia mtu, alipopata kwenda upande wa kidini, wanaojiita watu wa dini ulimwenguni. Kamwe hakujihusisha na madhehebu. Daima, aliyapinga, na akayapinga madhehebu ya siku hizo, na kuupinga utaratibu wa kidini wa siku hizo. Nionyeshe nabii mmoja, nionyeshe wakati mmoja katika Biblia, ambapo mtu yeyote wa Mungu aliwahi kukubaliana na zile zinazoitwa harakati za kidini za siku yake. Amina.

<sup>131</sup> Hata Eliya, baada ya kujenga shule ya manabii, mbona, alipopanda kule, wanataka aondoke. Alisema, “Ni pagumu sana hapa.” Mnaona? Ahabu na viongozi wa kidini wa siku zake; Eliya alijitenga, akaenda Mlima Karmeli.

<sup>132</sup> Angalieni Yohana Mbatizaji, akijitenga, hata hakwenda shuleni mwao, kujifunza theolojia yao. Lakini, Mungu alimtuma nyikani, kumtayarisha kwa ajili ya kazi fulani.

<sup>133</sup> Kundi la Kaini halijaweza kamwe kumvika mtu wa Mungu joho lao la kikanisa. Halitamwenea. Hiyo ni kweli. Angalieni, kote katika nyakati.

<sup>134</sup> Pia wakati Yesu alipokuja, kamwe hakushauriana na yeyote wa hao wanatheolojia, ila aliwaita, “Kundi la majoka, au nyoka nyasini.”

<sup>135</sup> Wanafunzi kamwe hawakukubaliana na lolote la madhehebu yao. Walikuwa upande wa Habili.

<sup>136</sup> Yusufu kamwe hakukubaliana nao. Alichukiwa na kukataliwa, kwa kusudi lile lile ambalo hao wengine walikataliwa. Kwa sababu, Mungu alikuwa pamoja naye katika njia ya kimbinguni, na kwa njia tofauti na ile aliyokuwa pamoja na hao wengine. Nao wakamchukia, bila sababu. Kaini alimchukia Habili, bila sababu. Wale ndugu walimchukia Yusufu, bila sababu.

<sup>137</sup> Na, siku hizi, ulimwengu wa kimadhehebu, haidhuru ni mkuu jinsi gani; ninavua kofia yangu na kusema, “Asante Mungu kwa ajili yao.” Lakini, katika mafundisho yao yote makuu, makanisa yao makuu, mambo makuu; bado, katika hayo yote, Mungu huwaita watu wasio na uhusiano wowote nayo, kwa maana hawatakubaliana na mambo ya kimbinguni. Kuna huduma inayoendelea, siku hizi; nao wanaichukia huduma hiyo, bila sababu.

<sup>138</sup> Nilimsikia mtu akisema hivi majuzi, ambalo karibu liigeuze damu yangu kuwa maji, kumsikia mtu mwenye ushawishi, mhubiri mashuhuri wa Kibaptisti.

<sup>139</sup> Naye alikuwa akisema, kwamba, si la Kimaandiko kwa mtu yeyote kumwabudu bikira Mariamu. Jinsi hilo lilivyo la kweli! Hiyo ni kweli. Alisema hakuna Maandiko, kumwabudu mtu yeyote ila Kristo. Hiyo ni kweli. Alisema, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, na ndani Yake ulikuwa utimilifu wa Uungu.” Hiyo ni kweli.

<sup>140</sup> Ndipo, baada ya mafundisho hayo yote mazuri, ya ajabu ya Maandiko, anageuka na kusema, “Kamwe hakuna muujiza uliopata kufanyika duniani.” Kwa sababu anaupinga kwa dhati uponyaji wa Kiungu, akageuka na kusema, “Kamwe hakukuwa na muujiza ulioopata kufanyika baada ya kifo cha Kristo. Hakuna mtu aliyewahi kuwafufua wafu, baada ya Kristo, kwa sababu Yeye Ndiye pekee aliyekuwa na Uzima wa Milele.”

<sup>141</sup> Lakini, nawaambieni, ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliwaambia wanafunzi Wake, “Enendeni mkaihubiri Injili; mkawaponye wagonjwa; na kuwafufua wafu; na kuwataka wenye ukoma.” Hivyo ndivyo Yesu alivyowaambia wanafunzi Wake.

<sup>142</sup> Watu wanawezaje kuwa vipofu hivyo kidini? Wanakuwa na mawazo finyu kwa sababu ya vizuizi vya kimadhehebu na kuwachukia ndugu zao, bila sababu. Mnalionga? Finyu sana, duni sana, wanafanya hivyo kwa sababu ya fahari yao kuu.

<sup>143</sup> Mhudumu mashuhuri wa nchi siku hizi, aliulizwa ni kwa nini hakuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, baada ya huo kuwasilishwa na watu wengine wa hadhi yake, ambao walikuwa wamepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Akasema, “Ingeidhuru huduma yangu.” Ukiniambia, wakati wowote . . .

<sup>144</sup> Inaweza kuidhuru huduma ya mtu binafsi, bali kamwe haitadhuru huduma ya Yesu Kristo ambayo itaendelezwa. Itaiendeleza huduma ya Yesu Kristo.

<sup>145</sup> Lakini huyu Bw. Daktari alisema ya kwamba hakuna mtu aliyewahi kufufuka katika wafu. Kasema, “Ninajua kuna kundi la watakatifu wanaojibingirisha nchini siku hizi, wanaodai ya kwamba wamewaona wafu wakifufuliwa. Lakini,” sema, “aha! Kamwe hakuna uthibitisho wa kisayansi wa uponyaji wowote au kitu kingine chochote.”

<sup>146</sup> Sasa, mnaona, hili hapa, ndugu yangu na dada yangu. Ninataka mliangalie hili kwa makini sana. Sababu yake, ni hii. Siku hizi, watu . . .

<sup>147</sup> Katika siku za Bwana Yesu, katika siku za Maagano, wakati watu walipomwamini Mungu, waliposikia juu ya kufanyika kwa muujiza, hawakujaribu kamwe kuuthibitisha kisayansi. Waliukubali. Waliamini tu, kwa maana walijua ya kwamba Mungu yupo.

<sup>148</sup> Lakini, siku hizi, kundi la makafiri limeingia katika huduma za kidini, naye anajaribu sana kuthibitisha mambo kisayansi.

<sup>149</sup> Basi hebu niseme jambo hili, linaposhuka kutoka Mbinguni, ninaamini, kwa moyo wangu. Hakuna wakati ambapo inaweza kuthibitishwa. Kwa sababu, kama ungeweza kumthibitisha Mungu, basi Yeye hakubaliwi tena kwa imani; ni ushahidi. Tunamwamini Mungu na miujiza Yake, kwa imani. Tunaviita vitu vile ambavyo havipo kana kwamba vipo, kwa sababu Mungu alisema hivyo; haijalishi ni nini.

<sup>150</sup> Ibrahimu hangeweza kuthibitisha kwamba mishipa ya maziwa ya Sara haikukauka. Hangeweza kuthibitisha kwamba—kwamba mirija, na kadhalika, ilitiwa mimba. Wao, angeweza... Hawangeweza kuthibitisha lolote la haya. Hawangeweza kuthibitisha labda, kwa majaribio ya mbegu, ya kwamba zilikuwa zimerutubishwa. Lakini aliamini, hata hivyo, na kukataa chochote kilichokuwa kinyume chake, na kuviita vile vitu ambavyo havikuwepo kana kwamba vilikuwapo. Kwa sababu, ndani ya pazia, tumaini la Mungu lilitulia juu ya Neno la Mungu, na kuviita vitu hivyo, viwe ni vya kisayansi au la, “Kweli, kwa sababu Mungu alisema hivyo.” Haya basi.

<sup>151</sup> Tunaamini. Kwa imani tunaipokea. Lakini, kama huyo ndugu, sio kubishana naye, siamini katika jambo hilo. Lakini laiti ndugu huyo angesoma jinsi Paulo alivyopigwa mawe mpaka kufa, nao watakatifu wakasimama juu yake na kuomba mpaka uhai ukamrudia. Jinsi ambavyo Paulo alihubiri usiku kucha, usiku mmoja, ndipo mtu fulani akaanguka kutoka kwenye orofa na kujiua, kijana; naye Paulo akaulaza mwili wake juu yake, ndipo Roho ya uzima ikarudi ndani yake tena. Jinsi Eliya alivyomfufua mtoto mchanga wa mwanamke mmoja baada ya kufa, hata miaka mia nane kabla ya Kuja kwa Kristo. Watu, hata bila baraka ya Roho Mtakatifu, walifanya miujiza ambayo jamaa hawa wanaogopa kushambulia kwa Roho Mtakatifu. Jamani, jamani! Ni jambo la kusikitisha jinsi gani!

<sup>152</sup> Kwa nini? Ni kwa sababu wana kiburi, nao wanawachukia ndugu zao, bila sababu; kama tu vile Yusufu alivyochukiwa, bila sababu. Mnaiona? Alichukiwa. Si kwa sababu alistahili kuchukiwa; kwa sababu, bila sababu. Hawakumwamini. Alikuwa akiishi katika milki nyingine.

<sup>153</sup> Nami ninasema hivi, sasa, kwa kuwa wakati wetu unazidi kuwa mfupi. Nasema hivi kwa ukweli wote wa moyo. Wanalichukia Kanisa, siku hizi, ambalo lina mambo ya kimbinguni. Ni wivu. Ni wivu wa rejareja, nao upo miongoni mwa wanadamu.

<sup>154</sup> Wanafunzi walikuwa nao. Walijionea aibu sana! Kwa sababu, siku kumi kabla, Mungu aliwapa uwezo wa kuwaponya wagonjwa, na kutoa pepo, na kuwafufua wafu. Nao walikuwa na mvulana mwenye kifafa mbele yao, nao walikuwa wameshindwa. Naye Yesu, aliposhuka kutoka mlimani, na kumponya mvulana huyo. Basi walimwuliza, “Je, kwa nini

hatukuweza?” Yeye hakusema, “Ni—niliwanyang’anya Nguvu Zangu.” Alisema, “Nawapa Nguvu.” Ninakuonyesha mahali alipozipa Kanisa, lakini huwezi kunionyesha mahali alipowahi kuwanyang’anya. Unaona? Yesu aliweka Maneno Yake ya uchaji juu ya nini? “Kwa sababu ya kutokuamini kwenu.”

<sup>155</sup> Ndipo basi, siku chache baadaye, walikutana na mtu ambaye hakuwa katika milki yao ya kikanisa. Alikuwa amemsikia Yesu akiyatamka mambo haya, naye alikuwa kazini. Alikuwa akitoa pepo. Ndipo Petro na Yohana wakaja kumwambia ilimpasa kuwa wa kundi lao la sivyo hangeweza kufanya hivi. “Itakulazimu kufuatana nasi na kuungana nasi. Sisi ndio kanisa, nawe huna budi kufanya hivyo!” Aliwashauri washike lao. Alikuwa akiendelea vizuri sana bila kujiunga na shirika lao.

<sup>156</sup> Kwa hiyo, kama maskini mambo madogo ya kitoto, kama tulivyo nayo siku hizi; maskini mawazo madogo, ya kitoto, walirudi mbio na kusema, “Tulimwona, naye alikuwa akitoa pepo.” Basi ilikuwa ni nini? Walikuwa na wivu kwa sababu alikuwa akifanya kile ambacho wasingeweza kufanya. Walikuwa wamekuwa wa kimwili. Macho yao, ya ufahamu wao, yalikuwa kama ya nduguze Yusufu, yalikuwa hayajaangaziwa, kwa hiyo wakarudi na kumfokea, na kumwambia Yesu.

<sup>157</sup> Naye Yesu akasema, “Mwacheni.” Amina. “Anafanya kazi nzuri. Anafanya kile nilichowaamuru kufanya, nanyi mmeshindwa kukifanya.” “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

<sup>158</sup> Kwa hiyo sasa, ndugu zangu wapendwa Wamethodisti na Wabaptisti na Wapresbiteri, kwa sababu mnafikiri lazima lipitie kanisani mwenu, Mungu anaweza kutoka kwa watakatifu hawa wanaojibingirisha kumwinulia Ibrahimu mawe. Hiyo ni kweli. Atakuwa na mtu ambaye atafanya kazi Yake. Hiyo ni kweli. Pamoja na kushindwa kwao kwote na makosa yao yote ya kijinga na kadhalika, wanayofanya, Israeli walifanya jambo lile lile, bali Uzoa huo wenye haki unasonga mbele.

<sup>159</sup> Nina furaha sana naweza kusema mimi ni mmoja wao. Kwa neema ya Mungu, leo, sisi ni mmoja wa hao. Nina furaha sana kwake, nanyi je? Moyo wangu unafurahi, mwanzoni mwa mwaka huu mpya, kujua kwamba Mungu, kupitia neema Yake ya ajabu, ameliweka jina langu katika Kitabu cha Uzima, kunipa ufahamu kwamba ninahusishwa miongoni mwa watu Wake waliofukuzwa. Na, pamoja na wanafunzi, naweza kusema hivi, ninayahesabu kuwa ni majaliwa kubeba lawama ya Jina Lake. Naam, bwana. Nina furaha sana kwamba mimi ni mmoja wao.

<sup>160</sup> Na sasa tunaanza hapa na Yusufu, kwenye ibada ijayo, ambayo inaweza kuwa usiku wa leo ama Jumatatu usiku, mojawapo, maana muda wetu umekwisha.

<sup>161</sup> Lakini, ninampenda. Je, hamumpendi? Yeye ni wa ajabu. Nami nina furaha sana leo kwamba ninaweza kushikana



mikono na safu hiyo ndefu ya waliodharauliwa na kukataliwa, na kuchukiwa na makasisi nchini kote. Hawa hapa. Wao ni duni. Hiyo ni kweli. Makasisi, tukizungumza juu ya ulimwengu, kielimu, na tukinena kijamii, wako juu yao. Nasi tuna furaha kuwa wanyenyekevu. Kwa sababu, wale ambao watajinyenyekeza, Mungu siku moja atakuja mara ya pili, katika Utukufu, kuliinua Kanisa Lake. Hadi wakati huo, “Hebu na tuishindanie kwa bidii Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.”

Na tuombe.

<sup>162</sup> Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kungekuwako na mtu mmoja asubuhi ya leo, ama wengi, natumaini, ambao bado hawajamkubali huyu Kristo, na baraka Zake kuu na nguvu Zake kuu. Na tunashangaa, leo, kama ungefanya chaguo lako leo, na kusema, “Bwana Yesu, ni mimi. Nami natamani kuwa mtumishi Wako, kwa moyo wangu wote, kushika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Ninaona sasa, Bwana, si kile ambacho ulimwengu unazungumzia; ni kile ambacho Biblia Yako inazungumzia. Si kile ulimwengu unachoniita. Wananichukia, kama walivyomchukia Yusufu. Wananichukia, kama walivyomchukia Habili. Wananichukia, kama walivyomchukia Yohana. Wananichukia, kama walivyomchukia Danieli. Wananichukia, kama walivyomchukia Ezeieli, kama Zekaria. Wananichukia, kama walivyomchukia Yesu. Wananichukia kama walivyowachukia Mitume na wale waliokufuata Wewe, bila sababu. Bwana, ninawaomba.”

<sup>163</sup> Umewahi kupata ujuzi kama huo, kwamba umetoka? “Nasi ni ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, tukimtolea Mungu dhabihu za kiroho; yaani, matunda ya midomo yetu, tukimpa sifa.” Je, ungeweza kusimama katikati ya ulimwengu wenye matatizo? Je, ungeweza kusimama mbele ya bosi wako? Je, ungeweza kusimama kwa unyenyekevu moyoni mwako, na upendo moyoni mwako, kwa ajili ya wenye dhambi wa ulimwengu huu, pamoja na Uzima wa Kristo ndani yako, na kutoa ushuhuda na sifa kwa utukufu wa Mungu? Ikiwa huna ujuzi huo, kwa nini usianze ulimwengu, maisha, kila kitu upya, leo, kwa kumwinulia Yeye mkono wako, na kusema, “Mimi sasa, Bwana, ninalikubali hilo, nami nataka Wewe unipe ubatizo wa Roho.”

<sup>164</sup> Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, Kanisa dogo asubuhi ya leo linasimama, tunajua, likionewa, likishambuliwa, adui amelidhulumu, akitupa mishale yake. Nasi tunaziomba nafsi zao zenye dhambi, Bwana. Hawajui kwamba wamepofushwa na mungu wa dunia hii.

<sup>165</sup> Kanisa, kwa ujumla, kote ulimwenguni leo hii; adui, watu wa kidini, wamewatupa kila mishale. Lakini licha ya hayo yote,

ule uamsho mkuu unaendelea. Maelfu ya watoto wanyenyekevu, maskini, waliopuuzwa wameingia katika maeneo haya kwa bahati, na kuuona mkono Wako wa kimiujiza, wamejazwa na Roho Mtakatifu. Nao si wa ulimwengu huu tena. Wao ni wasafiri na wageni. Hawaujali ulimwengu, bali wanatafuta Mji ujao, ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Wameziona nguvu Zako za uponyaji, za kuwaponya wagonjwa, ishara Zako na maajabu yatakayotendwa miongoni mwa watu Wako. Mambo makubwa hutokea, licha ya maeneo wanayolihukumu na kujaribu kulifinyilia chini. Watumishi Wako wanaingia tu moja kwa moja na kuanzisha uamsho, nao wanafagilia wanyenyekevu kwenye Ufalme wa Mungu.

<sup>166</sup> Katikati yetu asubuhi ya leo, tuna majaliwa ya kuwa na wamishenari hawa wanaoondoka kwenda nchi zingine.

<sup>167</sup> Mmoja, akiondoka kwenda Israeli. Ee Mungu, hiyo hapo. Mimina Roho Wako, kwake, Bwana. Na jalia mambo makubwa yatimizwe, na kuwafanya maskini Wayahudi hao wanaotangatanga warudi. Jalia wampokee Roho Mtakatifu, kama baba zao walivyofanya hapo mwanzo.

<sup>168</sup> Huyu hapa ndugu anayekwenda Kuba, huko visiwani. Ulisema, "Mpaka miisho ya dunia."

<sup>169</sup> Kitu fulani kinavuta, kinaivuta mioyo ya ndugu hawa. Wanayaacha makazi yao, wapendwa wao, bila kujali anasa na burudani za ulimwengu huu, bali kwenda katika nchi kame huko ng'ambo; chini ya mpinzani, akijaribu kuisimamisha kazi. Lakini kama tu vile yule maksai aliyeurudisha ule mkokoteni, uliozibeba zile amri, pamoja na lile sanduku la agano. Waliwaacha watoto wao, wakipiga kelele, nao wakashuka barabarani, wakiteremka, wakiimba, wakashuka kwenye Mwamba.

Tunakushukuru kwa ajili ya kila mhudumu.

<sup>170</sup> Tunamwona Ndugu John, ameketi huko nyuma katika kusanyiko letu, asubuhi ya leo, pia, kutoka Ujerumani. Jinsi alivyolelewa, maskini. Alikokota mkokoteni mdogo nchini, akihubiri Injili. Tunakushukuru kwa ajili yake!

<sup>171</sup> Na hawa vijana, na wahudumu wengine ambao wameketi karibu, na walei wote. Nilipouliza, Baba, nikiamini ya kwamba chini ya wakati kama huu, kwamba ikiwa mwanamume au mwanamke hakuwa na Kristo moyoni mwao, wangelinua mkono wao, hakika, wakiona uthibitisho wote wa Injili, kwamba Wewe ni yeye yule na Kanisa Lako ni lile lile.

<sup>172</sup> Ninakushukuru kwa ajili ya kila mtu. Ninaomba ya kwamba utawabariki. Na uwaponye miili yao ikiwa ni wagonjwa, na uwajalie shauku za moyo wao. Tujalie hili, Baba, tunaomba katika Jina la Yesu.

173 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu tutafakari tu dakika chache. Iweni tu katika maombi, kwa upole.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa  
Roho Mtakatifu,  
Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa  
kama mwanamume;  
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,  
Alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa watu  
kutoka dhambini.

Ndipo wakampiga mawe Stefano, alihubiri  
dhidi ya dhambi,  
Wao, wakiwa wamekasirika sana,  
wakakiponda-ponda kichwa chake;  
Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,  
Ndipo akaenda kujiunga na hao wengine, lile  
jeshi linalotoa uhai.

Kulikuwako Petro na Paulo, na Yohana  
mtauwa,  
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate  
kuangaza;  
Walichanganya damu yao, kama manabii wa  
kale, (Huo ungali ni ule Uzao, unaoteswa.)  
Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate  
kuhubiriwa kwa uaminifu.

Kulikuwako na nafsi chini ya madhabahu,  
wakilia, "Hata lini?"  
Bwana apate kuwaadhibu wale waliofanya  
makosa;  
Lakini kutakuwako na wengine  
watakaomwaga damu ya uhai wao,  
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na  
mafuriko Yake mekundu sana.

Inaendelea kudondoka damu, naam,  
inadondoka damu,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,  
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya  
Kweli,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

174 [Ndugu Branham anavumisha, *Inadondoka Damu*—Mh.]

175 Ee Mungu! Njoo, Bwana Yesu! Tufinyange sasa wakati tukiwa wanyenyekevu mbele zako. Ondoa kutokujali kwote maishani mwetu, kutoka mioyoni mwetu, wakati u—utamu wa Roho unaonekana kutia macho rangi. Mungu akilichukua Neno Lake sasa na kulitia maji. Tuna furaha sana kwamba umetujumuisha, Baba, kuwa wachukuzi wa Injili.

176 Tunaombea kila haja ya kanisa. Tunamwombea mchungaji wetu mpendwa, Ee Mungu; mtumishi mwaminifu, kamwe

hachoki, sikuzote tayari kwenda. Nena na moyo wake, leo hii, na umjulishe ya kwamba kuna thawabu kubwa inayongoja huko kwa ajili ya wachungaji hao waaminifu watakapokusanyika huko ng'ambo pamoja na wote waliokombolewa.

<sup>177</sup> Wabariki wachungaji wengine, na wamishenari, na washiriki wa Mwili wa Kristo, kila mahali. Utusamehe kupungukiwa kwetu, Bwana.

<sup>178</sup> Na sasa kama kuna haja mioyoni mwetu, Bwana, hivi Wewe, wakati ukiwepo, utatubariki? Kama kuna magonjwa katikati yetu, Bwana, huenda mtu fulani, ambaye amekuja katika kanisa hili dogo leo, nao wanatazama huko ng'ambo na kuona Kalvari, wanaona pale ulipo ule Uzao halisi. Ambapo Shetani alifikiri angeweza kumwangamiza kwa mauti, bali Mungu akamfufua tena. Kamwe hawezi kumwangamiza! Mungu ametoa ahadi, naye Mungu hudumu na ahadi Yake. Na kila ahadi ni ya kweli. Ulituahidi Uzima wa Milele, nasi tunao. Tunauhisi. Kuna kitu Fulani ndani yetu, kinachotembea, ambacho hatuwezi kukieleza. Ee Mungu! Katikati ya shida, tunahisi kitu Fulani kinachoshikilia huko ng'ambo "Kaeni tu kimya." Dhoruba zinaweza kuipiga hiyo Mbegu, meli inaweza kutikisa maskini gome letu. Utafanya njia ya kupitia juu, chini, kando-kando, au kupitia kwake, kwa njia fulani. Kwa hiyo, tumekaa moja kwa moja dhidi ya Neno, Bwana.

<sup>179</sup> Ninaomba sasa ya kwamba kama mtu fulani ni mgonjwa mkutanoni, kwamba Roho huyu, ambaye yumo humu jengoni sasa hivi, ashuke kwa upendo mkubwa, aseme, "Mtoto Wangu, huyu ni Mimi. Mimi ndimi Baba niliyekuumba. Mimi Ndimi niliyetoa e—elementi ardhini, zilizokufanya ulicho wewe. Shetani anajaribu kuingilia kazi Yangu. Chukua ahadi yangu, ewe mtoto."

<sup>180</sup> Na maombi haya ya imani ninatoa, nikiamini ya kwamba Wewe uko hapa. Jalia mikono Yako, Bwana, inyoshwe kwa kila moyo, na magonjwa yawaondokee watu. Namkemea ibilisi; ibilisi wa mateso, ibilisi wa hofu, ibilisi wa magonjwa ya kila namna. Wewe umesema, "Katika Jina Langu watatoa pepo." Katika umoja wa kanisa hili, na Roho hii asubuhi ya leo, tunatupilia mbali kila uovu kutoka kwa watu; tupate kuondoka hapa, tukiwa safi, kwa Dhabihu ya Bwana Yesu, tunapoikubali kwa unyenyekevu.

<sup>181</sup> Utubariki katika shughuli zijazo. Utubariki katika chochote tunachofanya. Nenda pamoja na wahudumu na wainjilisti na wamishenari, makwao, Bwana. Jalia siku moja kwamba tutakutana mi—miguuni Pako. Ndipo tutaweka nyara zetu chini. Mungu, watakuwa wa aina zote. Kutakuwako na mtu mweupe, mtu wa manjano, mtu mweusi. Wote pamoja, tutasema, "Bwana, hawa hapa." Hiyo itakuwa ni siku ya furaha iliyoje! Tujalie tufanye kazi kungali mchana, kwa maana usiku unakuja ambapo

hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Tunaomba baraka hizi katika Jina pe—pendwa la Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Amina.

Mambo yote yanawezekana, amini tu;  
Amini tu, amini. . . (Ni kitu gani?)  
Mambo yote yanawezekana, tu. . .

<sup>182</sup> Ni wangapi walikuwa na haja, na wangeweza kuamini sasa hivi? Utainua mkono wako, useme, “Sasa napokea.”

Sasa napokea, sasa napokea,  
Mambo yote yanawezekana, sasa napokea;  
Sasa napokea, sasa napokea,  
Mambo yote yanawezekana, sasa napokea.

<sup>183</sup> Sasa hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo sasa. Endelea tu, dada, kwenye piano, tafadhali. Utampokea?

<sup>184</sup> Unasema, “Ndugu Branham, nimekuwa mgonjwa kwa muda. Kumekuwa na kitu kilichoonekana kana kwamba nisingeweza kushinda. Nimeombewa, na watu binafsi.”

<sup>185</sup> Hilo ni zuri, ndugu, dada, lakini umewahi kufikiria ni nini? Ni ile ahadi ndogo ambayo umepewa. “Mambo yote yanawezekana kwake aminiye.”

<sup>186</sup> Je, hutalitupa hilo moja kwa moja katika Kalvari asubuhi ya leo? Shikilia tu mwisho wake hapa, Roho aliyekupa hiyo. Itupe moja kwa moja Kalvari, na kusema, “Hapo nanga yangu inashikilia. Sasa napokea, sasa hivi. Yote yamekwisha, sasa hivi. Haidhuru ni nini kitakachotukia, sasa hivi nanga yangu imeshikilia ndani ya pazia, nami ninapokea kile tu ninachoomba. Najua ninayo. Neno la Mungu lilisema hivyo. Na, Mungu, ninakutegemea Wewe sasa.” Labda ulikuwa na wasiwasi, shida za kifedha, chochote kile. Haidhuru ni nini, itupe moja kwa moja Kalvari.

Kwa kuwa mambo yote—mambo yote  
yanawezekana, amini tu.

<sup>187</sup> Ninaliacha tu lizame, kwa utamu sana. Si ni ajabu? Huu ni wakati wangu wa ibada. Neno limepandwa, unaona, sasa Mungu analitia maji. Hivi huwezi kuhisi hilo ninii. . . burudisho hilo, burudisho kutoka kwenye Uwepo wa Mungu, ukishuka tu chini, kuinyunyizia maji, useme, “Sasa, hapa, mtoto, na—naja na Neno Langu. Ninaliheshimu Neno Langu. Ninalilinda, mchana na usiku, na ninalimwagilia maji sasa moyoni mwako. Je, hamwezi kunichukua tu na kuniamini Mimi?”

Kwa maana mambo yote (Ati nini?)  
yanawezekana, amini tu.

<sup>188</sup> Jamani! Ajabu jinsi gani! Ni ajabu jinsi gani, kuzama tu ndani, kuhisi maji yakiitiririkia ile Mbegu! Ni kitu gani? Mbegu ya haki, imepandwa moyoni mwako. Ni Neno la Mungu. Hilo ndilo Mbegu. Huyu ni Roho Mtakatifu. Uzao ambao Mungu

aliahidi hapo mwanzo. Ninyi ni Uzao wa Ibrahimu, kwa kuwa wafu katika Kristo, na kuchukua Uzao wa Ibrahimu na ni warithi sawasawa na ile ahadi. Roho Mtakatifu alitoka kwa Uzao wa Ibrahimu, ambalo linawafanya ninyi wana na binti za Mungu.

<sup>189</sup> Sasa, huyo ni Roho Mtakatifu akiimwagilia maji hiyo ahadi uliyofanya muda mfupi uliopita, kwa ajili ya uponyaji wako, kwa ajili ya wokovu wako, kwa ajili ya mwenendo bora, hofu ipate kukuacha, kwa chochote unachohitaji; kwa safari hiyo ya kwenda visiwani, kwa safari hiyo ya nchi ya Israeli; kwa kanisa lako, kwa mahali pako, popote pale, nyumbani mwako. Huyo ni Roho Mtakatifu akisema, “Huyo ni Mimi. Niko pamoja nawe. Endelea. Ninaongoza njiani. Wewe, endelea tu kusonga mbele. Huyo ni Mimi.”

Kuna Asali Mwambani kwa ajili yako;  
Acha dhambi yako ifunikwe na Damu,  
Kuna Asali Mwambani kwa ajili yako.

Na tusimame.

Loo, nenda mitaani na barabara ndogo,  
Lihubiri Neno... (Una chochote unachotaka  
kusema?)

Mwambie kila ndugu aliyeanguka,  
Kuna Asali Mwambani kwa ajili yako.

Loo, kuna Asali Mwambani, ndugu yangu.  
Kuna Asali Mwambani kwa ajili yako;  
Acha dhambi zako zifunikwe na Damu,  
Kuna Asali Mwambani kwa ajili yako.

<sup>190</sup> Sasa, angalia, sitaki muondoke bado. Nataka umwangalie mtu anayesimama karibu nawe, akupe mkono, useme, “Mungu akubariki, ndugu,” au dada, yeyote yule. Geuka tu moja kwa moja. Hii ni maskini maskani ndogo isiyo na mipaka ya kimadhehebu. Tuko tu safarini mwetu, watu wa kipekee. Vema.

Peleka Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na wa majonzi;  
Litakupa furaha na faraja,  
Peleka kila uendako.

Jina la thamani, (Jina la thamani!), Lo ni tamu  
jinsi gani! (Lo ni tamu jinsi gani!)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa kila mtu aangalie huku sasa.

Tu—tukiliinamia Jina la Yesu,  
 Tukisujudu miguuni Pake,  
 Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa  
 wafalme,  
 Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Lo ni tamu  
 jinsi gani! (Lo ni tamu jinsi gani!)  
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
 Jina la thamani, (Jina la thamani!) Lo ni tamu  
 jinsi gani!

Tumaini la duniani na furaha . . . (...?...) )

<sup>191</sup> Sasa huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa Bwana Yesu. Imekuwa ni yubile kuu, karamu kuu, karamu ya kipentekoste juu ya Neno na mambo ya Mungu, juu ya Roho Wake Mtakatifu. Tunataka kuomba baraka za Mungu juu ya ndugu zetu wamishenari wanaoenda hudumani sasa, na Mungu awape safari njema moja kwa moja. Tunawapa ahadi; tutakuwa tukiwaombea, ndugu, na dada. Wake zao, wapendwa wao, wazieni yale ambayo wanawake hao wanapitia. Najua, kwa mke wangu mwenyewe.

<sup>192</sup> Kwa wachungaji hapa, Ndugu Jackson, na—na nadhani Ndugu Beeler yuko nyuma kule, na wachungaji wengine wengi. Teddy hapa nyuma, mhudumu kijana. Wengine wengi waliopo hapa, tunaomba tu baraka za Mungu. Ndugu mchanga hapa, kutoka huko chini katika church of God, ambaye tutamwona alasiri ya leo. Tunaomba baraka juu yake, mwinjilisti, naamini ndivyo alivyo. Sivyo, ndugu? Jina lako nani? [Ndugu huyo anasema, “Morgan.”—Mh.] Ndugu Morg- . . . [“Morgan.”] Morgan, Ndugu Morgan. Nina furaha sana kuwa nao wote hapa!

<sup>193</sup> Na, sasa, tunapomwinamishia vichwa vyetu, na tutazame. Kuna ndugu mdogo mnyenyekevu anayesimama nyuma ya jengo. Anakokota mkokoteni mdogo, nasikia, kote nchini. Wengi wao wanamfahamu kama “Nabii John.” Tunamwita “Ndugu John,” huku. Sikuzote nilimheshimu mtu huyo. Lakini, hivi majuzi nilikuwa nimewatembelea marafiki zangu wengine, hao ni ndugu. . . Dada Jimmy O’Neal, huko Sellersburg. Huyo ni mkwe wa Ndugu na Dada Green. Wapo asubuhi ya leo. Naye Ndugu John alikuwa amekuwa nyumbani kwao, nao wakaniambia jinsi alivyokuwa Mkristo muungwana halisi. Nao wakanisimulia maisha yake, yale aliyokuwa amewaambia, na jinsi alivyokuwa amepitia majaribu makali. Naye amepitia magumu. Nasi tutamwomba, asubuhi ya leo, kama ataliruhusu kusanyiko hili liondoke, na kuomba baraka zake kutoka kwa Mungu, juu ya kusanyiko hili. Je, utatufanyia hivyo, Ndugu Johnny? Wakati nyote mkiviinamisha vichwa vyetu. Basi, Ndugu John, naomba uturuhusu tufumukane katika maombi.



*YUSUFU AKIKUTANA NA NDUGUZE* SWA56-1230

(Joseph Meeting His Brethren)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 30 Desemba, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)



## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)